JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA KILIMO

BODI YA CHAI TANZANIA

IDARA YA HUDUMA ZA USIMAMIZI

# TAARIFA YA MNADA NAMBA 45 WA CHAI KUPITIA MFUMO WA KIDIGITALI - DOTA.

NOVEMBA, 2025

## TAARIFA YA WIKI YA MNADA WA CHAI NAMBA 45.

Mnada wa chai namba **45** ulifanyika tarehe **10 Novemba, 2025**. Jumla ya kilo **14,640** za chai ziliuzwa ambazo zilikuwa kwenye ghala la Kipawa. Chai iliuzwa kati ya dola za Marekani (USD) 1.3 hadi 1.6. Chai zote zilizouzwa zilinunuliwa na kampuni ya Afri Tea Coffee Blenders Ltd jedwali namba 1 linaonyesha chai zilizouzwa.

**Jedwali Na. 1:** Chai zilizouzwa mnada namba 45 kati ya minada 51 inayotarajiwa kufanyika mwaka 2025.

**Mzalishaji/ Kiwanda:** Mponde Tea Factory.
**Mnunuzi:** Afri Tea Coffee Blenders Ltd.
**Ghala:** Kipawa.

| Na | Aina ya chai/ Daraja | Idadi ya Mifuko | Kiasi (Kg) | Bei ya awali (USD) | Bei ya mauzo (USD) | Thamani (USD) | Thamani (TZS) | Hali |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **1** | PF1 | 40 | 2,520 | 160 | 160 | 4,032 | 9,902,511 | Imeuzwa |
| **2** | PF1 | 40 | 2,520 | 160 | 160 | 4,032 | 9,902,511 | Imeuzwa |
| **3** | PD | 40 | 2,800 | 165 | 160 | 4,480 | 11,002,790 | Imeuzwa |
| **4** | PD | 40 | 2,800 | 165 | 160 | 4,480 | 11,002,790 | Imeuzwa |
| **5** | FNGS | 40 | 2,000 | 132 | 130 | 2,600 | 6,385,548 | Imeuzwa |
| **6** | FNGS | 40 | 2,000 | 132 | 130 | 2,600 | 6,385,548 | Imeuzwa |
| **Jumla Kuu** | | **240** | **14,640** | | | **22,224** | **54,581,698** | |

## TAARIFA YA CHAI ILIYOPO KWENYE GHALA LA BODI YA CHAI KIPAWA

Kiasi kilichopo kwenye ghala la kipawa ni tani 69.645 sawa na gunia 1,199. Aidha tunaendelea kuwasisitiza wadau waendelee kuleta chai kwenye mnada kama *auction rule book* inavyo elekeza . Angalau asilimia 15% ya uzalishaji wa kila kiwanda kiuzwe kuitia mnada wa DOTA.

## MAELEZO YA KINA YA MAFANIKIO MNADA

Tangu kuanzishwa mnada wa kidigitali wa chai mwaka 2023 bei zimekuwa zikiimarika mwaka hadi mwaka. Na katika mnada Namba 45 imepatikana bei ya juu zaidi ambayo haijawahi kutokea ya **USD 1.60 kwa kilo** moja ya chai. Hii ni kutokana na **matokeo ya kazi kubwa inayofanywa na Serikali kupitia Wizara ya Kilimo na Bodi ya Chai Tanzania (TBT)** katika kusimamia ubora wa chai, kuimarisha mifumo ya minada ya chai, na kuhakikisha uwazi katika biashara ya chai.

Bodi ya Chai Tanzania imekuwa mstari wa mbele katika:


- **Kusimamia ubora wa chai** kuanzia hatua ya kilimo hadi uuzaji,
- **Kutoa elimu kwa wakulima** kuhusu uzalishaji bora na utunzaji wa mashamba,
- **Kuratibu minada ya chai kwa uwazi na ushindani**,
- **Kuhamasisha ushirikiano kati ya wadau** kama vile viwanda vya kuchakata chai, wanunuzi, na mawakala wa mauzo/madalali.
- Kuhamasisha wanunuzi wengi kushiriki mnada wa chai.

Kupitia juhudi hizo, mnada wa chai umekuwa mfano wa mafanikio ya sekta ya chai nchini, na bei ya **USD 1.60** inatoa matumaini mapya kwa wakulima na wadau wote kuwa sekta ya chai inakua.

**Jedwali linalooonesha:** Mwenendo wa Bei ya chai kupitia mnada wa kidigitali (DOTA) kwa Robo ya Pili 2025/2026.

| *Mnada Namba* | *Idadi ya Mifuko* | *Uzito (Kgs)* | *Bei (USC)* |
|---|---|---|---|
| ***29*** | 220 | 12,200 | 64 |
| ***30*** | 660 | 35,720 | 69 |
| ***31*** | 760 | 26,960 | 68 |
| ***34*** | 40 | 1,800 | 92 |
| ***35*** | 440 | 19,200 | 106 |
| ***40*** | 240 | 8,360 | 150 |
| ***42*** | 340 | 19,400 | 155 |
| ***45*** | 240 | 14,640 | 160 |
| ***Jumla*** | **2,700** | **123,640** | |

**Grafu inaonyesha:** Mwenendo wa Bei ya chai kupitia mnada wa kidigitali (DOTA) kwa Robo ya Pili 2025/2026.




**NINAOMBA KUWASILISHA** **IDARA YA HUDUMA ZA USIMAMIZI**

**11 Novemba, 2025**